# PBPA Bulletin

Toleo Na. 04 | Februari, 2026



PbpaTanzania

PbpaTanzania

pbpa_tanzania



# KAMATI YA UHARIRI

| | |
|---|---|
| Lilian Rwegimbura | MWENYEKITI |
| Sarah Mwakyusa | KATIBU |
| Matiko Sanawa | MJUMBE |
| Henry Kilenga | MJUMBE |
| Rehema Mahundi | MJUMBE |
| Nyamhoni Chacha | MSANIFU |


Wasiliana Nasi

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja
Sanduku la Posta 2634, Dar es Salaam,
Tanzania
info@pbpa.go.tz
+255 222 129 009
+255 222 129 009

# Yaliyomo

| | |
|---|---|
| NAIBU WAZIRI SALOME MAKAMBA AIPONGEZA PBPA KWA UTENDAJI BORA | 03 |
| WATUMISHI WA PBPA WATAKIWA KUZINGATIA MAADILI NA UBUNIFU KAZINI | 06 |
| ZIMBABWE YAPONGEZA UFANISI WA MFUMO WA BPS | 08 |
| PBPA YAFUNGUA MILANGO KWA VIJANA WA UHANDISI WA MAFUTA KUTOKA UDSM NA DMI | 11 |
| BANDARI YA MTWARA YAANDIKA HISTORIA MPYA KATIKA HUDUMA ZA MAFUTA YANAYOSAFIRISHWA KUELEKEA NCHI JIRANI (TRANSIT) | 13 |
| MFUMO WA UAGIZAJI MAFUTA KWA PAMOJA WAVUTIA WADAU ZITF | 14 |



# NAIBU WAZIRI SALOME MAKAMBA AIPONGEZA PBPA KWA UTENDAJI BORA

***Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba, akizungumza na viongozi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Wakala jijini Dar es Salaam.***

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba (Mb), ameipongeza Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa utendaji wake imara katika kuhakikisha Tanzania inakuwa na akiba ya mafuta ya kutosha na yenye viwango vinavyokidhi mahitaji ya taifa.

Alitoa pongezi hizo Desemba 6, 2025, alipotembelea ofisi za PBPA jijini Dar es Salaam na kufanya mazungumzo na Menejimenti ya Wakala huo.

Akizungumza na uongozi wa PBPA, Mhe. Makamba alisisitiza umuhimu wa wananchi kuelewa majukumu ya PBPA na mchango wake katika ustawi wa Sekta ya Nishati.

Alitoa wito kwa Wakala kuongeza juhudi za kutoa elimu kwa umma kuhusu kazi wanazozifanya, hasa kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya Mafuta katika uchumi wa nchi.

"Nawapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya, lakini hakikisheni mnatoa elimu kwa Watanzania kuhusu majukumu yenu na kazi zenu," alisema Mhe. Salome, akisisitiza kuwa uelewa wa wananchi ni sehemu muhimu ya kujenga imani na uwazi katika usimamizi wa Sekta ya Mafuta.

Mhe. Salome aliitaka PBPA kuongeza mchango wake katika kuwaandaa wazawa kushiriki kikamilifu katika sekta hiyo.

Alieleza kuwa ni muhimu kwa taifa kuwa na wawekezaji wa ndani walio na uwezo na ujuzi wa kushindana kwenye biashara ya mafuta, ili kuongeza ushiriki wa Watanzania katika uchumi wa nishati.

"Lazima tupate wawekezaji wa Tanzania; tuwawezeshe waingie kwenye hii biashara," alisisitiza Mhe. Salome.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa PBPA, Bw. Erasto Simon, alisema kuwa wakala umeendelea kuimarisha usalama wa nishati nchini kupitia usimamizi bora wa upatikanaji wa mafuta, ufuatiliaji sahihi wa takwimu za uingizaji wa bidhaa na kuwezesha Serikali kupanga mapato yake kwa uhakika.

Alisema mafanikio haya yamechangiwa zaidi na usimamizi thabiti wa Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (Bulk Procurement System – BPS), ambao umejipambanua kuwa chombo makini cha kuimarisha ufanisi katika Sekta ya Mafuta.

"Mfumo wa BPS umesaidia hata nchi za jirani kuagiza mafuta kwa takriban asilimia 95, sambamba na kudhibiti ubora wa bidhaa za mafuta zinazoingia au kupitia nchini," alisema Bw. Erasto Simon.

Aliongeza kuwa PBPA imekuwa kituo muhimu cha mafunzo na ushirikiano wa kikanda, ambapo mataifa kama Malawi, Zambia, Uganda, Rwanda, Zimbabwe na Namibia yamekuwa yakitembelea Tanzania kwa lengo la kujifunza mbinu bora zaidi za uagizaji wa mafuta kwa pamoja ili kuboresha mifumo yao ya kitaifa. Ziara hizi zimekuwa sehemu ya ukuaji wa diplomasia ya kiuchumi kupitia Sekta ya Nishati.

Alisema uwazi katika mchakato mzima wa uagizaji mafuta kuanzia tangazo la zabuni, ufunguaji, hadi uteuzi wa wazabuni umeendelea kuongeza uaminifu wa wadau na kuboresha ufanisi wa upatikanaji wa bidhaa nchini.

Ziara ya Naibu Waziri Salome ni sehemu ya utambulisho wake rasmi katika majukumu mapya ndani ya Wizara ya Nishati, pamoja na kujifunza kwa undani shughuli na majukumu ya PBPA kufuatia kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo. Ziara hiyo imezidi kuthibitisha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuimarisha mifumo ya usimamizi wa nishati, kuongeza uwazi, na kuendeleza ushiriki wa Watanzania katika Sekta ya Mafuta.



*Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti kutoka PBPA wakiwa katika kikao na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba, katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Wakala jijini Dar es Salaam.*




***Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Makamba akisikiliza maelezo ya utendaji kazi wa mfumo wa SCADA kutoka kwa Bw. George Shayo wakati wa ziara yake kwenye ofisi ya Wakala jijini Dar es Salaam.***



# WATUMISHI WA PBPA WATAKIWA KUZINGATIA MAADILI NA UBUNIFU KAZINI

***Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) Bw. Erasto Simon (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wakala baada ya kufungua mkutano huo uliofanyika mkoani Morogoro.***




Watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wameaswa kuzingatia maadili ya utendaji kazi, kuongeza ubunifu na kutekeleza majukumu yao kwa weledi ili kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi la PBPA kilichofanyika Desemba 13, 2025 mkoani Morogoro, Mwenyekiti wa Baraza hilo abaye pia ni Mtendaji Mkuu wa Wakala huo, Bw. Erasto Simon, alisema kuwa maadili na weledi ni nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya Taasisi.

"Ufanisi wa PBPA unategemea kwa kiasi kikubwa maadili ya

*"Ni muhimu wajumbe kujiandaa mapema ili kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unafanyika kwa uwazi na kwa kuzingatia matakwa ya kisheria,"*

watumishi wake, ubunifu katika kazi na uwajibikaji wa kila mmoja. Tunapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya Utumishi wa Umma ili kuleta matokeo chanya," alisema Simon.

Alifafanua kuwa PBPA inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya kazi kadri inavyowezekana, sambamba na kusimamia maadili ya watumishi ili kuhakikisha hakuna vitendo vinavyokiuka misingi ya kazi.

"Wakala umejipanga kuhakikisha mazingira ya kazi yanaboreshwa na maslahi ya watumishi yanazingatiwa, huku tukisimamia nidhamu na maadili ya kazi bila muhali," alisisitiza.

Aidha, Mtendaji Mkuu huyo alisema PBPA imeendelea kuajiri watumishi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu pamoja na kupata idhini ya kutumia miongozo mbalimbali ya kiutumishi.

"Tumehakikisha stahiki za watumishi zinalipwa kwa wakati na kwa mujibu wa taratibu, kwani tunatambua kuwa ustawi wa mtumishi ni msingi wa utendaji bora," aliongeza.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Bw. Issa Mwitazy aliwataka wajumbe wa baraza kujiandaa kikamilifu kwa ajili ya uchaguzi wa wajumbe wapya wa Baraza la Wafanyakazi, unaotarajiwa kufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Sura 105 na Kanuni zake za Mwaka 2005.

"Ni muhimu wajumbe kujiandaa mapema ili kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unafanyika kwa uwazi na kwa kuzingatia matakwa ya kisheria," alisema.

Baraza la Wafanyakazi ni jukwaa muhimu la kisheria la ushirikishwaji kati ya uongozi na watumishi, linalokutana angalau mara mbili kwa mwaka, likiwa na lengo la kujadili masuala ya ustawi wa watumishi na kuboresha utendaji kazi wa taasisi.







***Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja wakimsikiliza Mtendaji Mkuu Bw. Erasto Simon (hayupo pichani) wakati akifungua mkutano wa Baraza hilo uliofanyika mkoani Morogoro.***

# ZIMBABWE YAPONGEZA UFANISI WA MFUMO WA BPS




***Meneja wa Udhibiti kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati nchini Zimbabwe (ZERA), Bw. Learnmore Nechitoro, (katikati) akifuatilia ufunguzi wa zabuni ya Ununuzi wa Mafuta kupitia mfumo wa BPS uliofanyika katika ukumbi wa mikutano Ofisi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) jijini Dar es Salaam.***

Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati nchini Zimbabwe (ZERA) imepongeza Wakala ya Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa kusimamia kwa ufanisi, uwazi na ubunifu Mfumo wa Uagizaji Mafuta nchini Tanzania.

Hayo yamesemwa na Meneja wa Udhibiti kutoka ZERA, Bw. Learnmore Nechitoro, alipofanya ziara ya kikazi na Wajumbe wengine 13 kwenye ofisi ya PBPA jijini Dar es Salaam na kufurahishwa namna PBPA inavyotekeleza mfumo wa BPS ambao kwa sasa unaaminika kama moja ya mifumo bora zaidi barani Afrika.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Bw. Nechitoro alisifu PBPA kwa kusimamia mfumo wenye kiwango cha juu cha uwazi, kuanzia hatua ya kupokea zabuni, kuzifungua mbele ya wadau, hadi mchakato wa ushindanishaji ambao umejijengea imani ya kikanda.

Alisema kuwa umahiri ulioshuhudiwa umeonyesha kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika uadilifu na ufanisi wa Sekta ya Mafuta, na kwamba ZERA itaenda kutumia maarifa hayo kuboresha mifumo yao ya udhibiti nchini Zimbabwe.

"Tumejifunza mengi, si tu kuhusu mchakato mzima wa zabuni, bali pia namna ambayo PBPA imejenga mfumo wenye ushindani wa karibu katika viwango

vya bei, jambo ambalo linapelekea kupatikana kwa gharama nafuu kwa taifa. Uwazi huu ni darasa muhimu kwetu kama wadhibiti," alisema Nechitoro.

Mbali na kutembelea ofisi za PBPA, ujumbe huo ulipewa fursa ya kushuhudia moja kwa moja hatua muhimu za usimamizi wa zabuni, ikiwa ni pamoja na mchakato wa kufunga na kufungua zabuni na namna wazabuni wanavyopimwa kwa kuzingatia ushindani wa kimataifa.

Maafisa hao walisema kuwa mfumo wa BPS umekuwa mfano bora wa utekelezaji wa sera zenye tija, na kwamba mafanikio hayo yanatoa dira mpya kwa mataifa mengine ya Afrika Mashariki.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo , Mtendaji Mkuu wa PBPA, Bw. Erasto Simon alisema kuwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015, PBPA imebadilisha sura ya usalama wa nishati nchini kwa kuongeza utulivu wa soko, kuimarisha bei, na kujenga mfumo wa uwazi unaoaminiwa na wadau wote.

Alifafanua kuwa Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja umeiwezesha Tanzania kutumia nguvu ya ununuzi wa Pamoja, hivyo kupata bei shindani, kupanga ratiba za meli kwa usahihi na kuongeza ufanisi katika upakuaji wa bidhaa za petroli.

"Uwazi huu umeongeza imani ya wadau na wananchi kuhusu namna Sekta ya Mafuta inavyosimamiwa, na kupunguza malalamiko ambayo hapo awali yalikuwa yakijirudia mara kwa mara," alisema Simon.

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania PBPA imeendelea kuwa kitovu cha ushirikiano wa kikanda. Nchi kutoka kanda mbalimbali, zikiwemo Zambia, Msumbiji, Namibia, Uganda, Rwanda, Zimbabwe na Burundi, tayari zimetembelea PBPA kwa lengo la kujifunza mbinu za uendeshaji wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja. Baadhi ya mataifa haya tayari yameanza kutumia mbinu walizojifunza kuboresha upatikanaji wa mafuta katika masoko yao.

Ziara ya ujumbe wa ZERA ni ushahidi kwamba PBPA inaendelea kuipa Tanzania hadhi kubwa kimataifa kupitia ufanisi, teknolojia na usimamizi makini wa Sekta ya Mafuta sekta ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa na maendeleo ya jamii.



***Baadhi ya Wajumbe kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati nchini Zimbabwe (ZERA) wakishuhudia ufunguzi wa zabuni ya Ununuzi wa Mafuta kupitia mfumo wa PBPS uliofanyika katika ukumbi wa mikutano Ofisi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) jijini Dar es Salaam.***

*"Uwazi huu umeongeza imani ya wadau na wananchi kuhusu namna Sekta ya Mafuta inavyosimamiwa, na kupunguza malalamiko ambayo hapo awali yalikuwa yakijirudia mara kwa mara"*




*Picha ya pamoja ya Wajumbe kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati nchini Zimbabwe (ZERA) na Wataalamu kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) baada ya kikao.*

# PBPA YAFUNGUA MILANGO KWA WANAFUNZI WA UHANDISI WA MAFUTA KUTOKA UDSM NA DMI

Wanafunzi 30 wa Kitivo cha Uhandisi wa Petroli na Gesi (Petroleum Engineering) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), chini ya Jumuiya ya Wahandisi wa Mafuta (SPE), wametembelea Ofisi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa lengo la kujifunza kwa vitendo.
Akizungumza wakati wa ziara hiyo iliyofanyika tarehe 30 Januari, 2026, Kaimu Meneja Sehemu ya Uagizaji Mafuta na Lojistiki za Petroli PBPA, Mhandisi Sophia Kidimwa, alisema kuwa wanafunzi hao wamepata fursa ya kuelewa mchakato mzima wa upatikanaji wa mafuta nchini kuanzia hatua za uagizaji hadi usimamizi wa lojistiki za kupokea mafuta.

“Tumepokea ugeni wa wanafunzi wa mwaka wa nne kutoka UDSM na DMI waliokuja kujifunza kuhusu taratibu zote za upatikanaji wa mafuta hapa Tanzania, jinsi mafuta yanavyoingia nchini, mchakato mzima wa uletaji wake pamoja na lojistiki za kupokea mafuta na manufaa ya Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS),” alisema Sophia.

Aliongeza kuwa PBPA imekuwa ikipokea wageni kutoka taasisi mbalimbali zinazopenda kujifunza kuhusu mfumo wa BPS kutokana na mafanikio na manufaa yake kwa Taifa.

“Kama taasisi, tumekuwa tukitoa uelewa huo kwa wageni wetu na wamekuwa wakionyesha kuridhika. Tunaendelea kuwakaribisha wadau wote wanaopenda kujifunza kuhusu Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja,” alisisitiza.

Kwa upande wake, Mhandisi kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Prudence Laurean, alisema wanafunzi hao walipitishwa katika mifumo yote ya PBPA kuanzia hatua za uagizaji wa mafuta hadi mafuta yanapofika kwenye maghala ya kuhifadhia, ikiwemo matumizi ya Mfumo wa SCADA katika ufuatiliaji wa mafuta wakati wa kushushwa kutoka melini kwenda kwenye maghala ya Serikali na binafsi.

“Mafunzo haya ni muhimu sana kwa wanafunzi kwani yanawajengea uelewa wa kina kuhusu kazi za PBPA na faida zitakazowasaidia kitaaluma hapo baadaye,” aliongeza.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi, Sifrina John, mwanafunzi wa mwaka wa nne Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema ziara hiyo imelenga kuwaunganisha wanafunzi na uhalisia wa kazi katika sekta ya mafuta nchini.

“Lengo letu ni kuunganisha yale tunayojifunza darasani na mazingira halisi ya kazi katika sekta ya mafuta, na kuelewa kwa vitendo jinsi PBPA inavyofanya kazi katika uagizaji na usimamizi wa ugavi wa mafuta nchini,” alisema Sifrina.

Aliongeza kuwa wanafunzi wamefurahishwa na mafunzo waliyoyapata na namna PBPA inavyosimamia ugavi wa mafuta pamoja na mchango wake katika uchumi wa Taifa.

“Tumepata uelewa wa kina kuhusu mchakato wa uagizaji wa mafuta, usimamizi wa ugavi na mchango wa PBPA katika uchumi wa nchi. Mafunzo haya yametujenga kwa kiasi kikubwa kwa kuunganisha nadharia na vitendo,” alisisitiza.

Ziara hiyo ni mwendelezo wa juhudi za PBPA katika kuimarisha ushirikiano na wadau kutoka taasisi mbalimbali nchini sambamba na kukuza uelewa wa vijana kuhusu mifumo ya kimkakati inayosimamia sekta ya mafuta na mchango wake katika uchumi wa Taifa.



Mhandisi Prudence Laurian akielezea utendaji kazi wa mfumo wa SCADA kwa Wanafunzi wa Kitivo cha Uhandisi wa Petroli na Gesi (Petroleum Engineering) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), chini ya Jumuiya ya Wahandisi wa Mafuta (SPE)



Kaimu Meneja Sehemu ya Uagizaji Mafuta na Lojistiki za Petroli PBPA, Mhandisi Sophia Kidimwa, akizungumza na Wanafunzi wa Kitivo cha Uhandisi wa Petroli na Gesi (Petroleum Engineering) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), chini ya Jumuiya ya Wahandisi wa Mafuta (SPE), (hawapo kwenye picha).



Picha ya pamoja ya Wataalamu wa PBPA na Wanafunzi wa Kitivo cha Uhandisi wa Petroli na Gesi (Petroleum Engineering) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), chini ya Chama cha Wahandisi wa Mafuta (SPE).



# BANDARI YA MTWARA YAANDIKA HISTORIA MPYA KATIKA HUDUMA ZA MAFUTA YANAYOSAFIRISHWA KUELEKEA NCHI JIRANI (TRANSIT)

Bandari ya Mtwara imeendelea kuthibitisha uwezo wake wa kiutendaji baada ya kupokea meli MT CL MARGARETH iliyobeba tani 28,725.387 za mafuta ya petroli, hali inayoashiria mabadiliko makubwa ya kimkakati katika matumizi ya bandari mbadala nchini na hivyo kuongeza ufanisi katika bandari ya Dar es Salaam.

Akizungumza kuhusu mafanikio hayo, Mhandisi Moses Nyaronga kutoka PBPA alisema kuwa kushusha mafuta yanayosafirishwa kuelekea nchi jirani (transit), kwa kiasi kikubwa kupitia Bandari ya Mtwara kumeleta tija kubwa katika mifumo ya uagizaji mafuta kwa Pamoja.

"Kushusha mafuta kwa kiasi kikubwa kwa wakati mmoja kupitia Bandari ya Mtwara kumeongeza ufanisi kupitia kupunguza muda wa meli kukaa bandarini na kupunguza msongamano wa meli katika Bandari ya Dar es Salaam hivyo kupunguza gharama za uletaji mafuta nchini," alisema Nyaronga.

Alieleza kuwa mpango huo umeimarisha usalama wa ugavi wa mafuta kwa kupunguza utegemezi wa bandari moja, sambamba na kuboresha usimamizi wa shehena za mafuta yanayosafirishwa kuelekea nchi jirani (transit).

Kwa upande wake, Bw. Ferdinand Nyathi Meneja wa Bandari ya Mtwara, alisema kuwa Bandari ya Mtwara imeanza rasmi kupokea na kuhudumia meli za mafuta yanayosafirishwa kuelekea nchi jirani tangu mwezi Septemba , 2025, hatua ambayo imefungua ukurasa mpya wa kibiashara katika bandari hiyo.

"Awali Bandari ya Mtwara haikuhudumia mafuta yanayosafirishwa kwenda nchi jirani, lakini kutokana na maboresho ya miundombinu na mifumo ya utoaji huduma, sasa meli za mafuta zinaendelea kuwasili na bandari imekuwa kivutio kipya kwa masoko ya nchi zisizo na bandari," alisema Bw. Nyathi .

Aliongeza kuwa katika kuimarisha ufanisi wa huduma, muda wa kushusha mafuta umepungua kwa kiwango kikubwa, ambapo kwa sasa shughuli hiyo huchukua kati ya siku mbili hadi nne kulingana na ukubwa wa meli, ikilinganishwa na siku saba zilizokuwa zinahitajika hapo awali.

Wadau wa bandari waliohudhuria hafla ya mapokezi ya meli hiyo Mkoani Mtwara walipongeza Serikali kwa ushirikiano na juhudi za makusudi katika kujenga mazingira rafiki ya biashara.

# MFUMO WA UAGIZAJI MAFUTA KWA PAMOJA WAVUTIA WADAU ZITF




***Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mhe. Queen Sendiga, akiwa na Watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) alipotembelea banda katika maonesho ya 12 ya Biashara ya Kimataifa ya Zanzibar (ZITF) yaliyofanyika viwanja vya Dimani, Zanzibar.***

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) unaendelea kupanua wigo wa elimu ya nishati kwa wananchi na wadau kupitia ushiriki wake katika Maonesho ya 12 ya Kimataifa ya Biashara ya Zanzibar (ZITF) yaliyofanyika katika Viwanja vya Maonesho Fumba, Zanzibar.

Ushiriki huo ulivutia idadi kubwa ya wananchi, wafanyabiashara na wadau wa sekta ya nishati waliotembelea banda la PBPA kupata elimu na ufafanuzi kuhusu Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja na mchango wake kwa uchumi wa taifa.

Wakizungumza wakati wa maonesho hayo, maafisa wa PBPA walieleza kuwa lengo kuu la ushiriki wao ni kuhakikisha wananchi wanaelewa nafasi ya

mfumo wa uagizaji wa pamoja katika kulinda maslahi ya taifa na kuchochea uthabiti wa uchumi, sambamba na kuondoa dhana potofu kuhusu mienendo ya bei za mafuta.

Ushiriki wa PBPA katika ZITF ulipata heshima kubwa kufuatia ziara ya Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Mwanaasha Khamis, aliyetembelea banda la wakala huo na kupongeza juhudi zinazofanywa katika kusimamia mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja kwa uwazi na weledi.

"Mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja unaosimamiwa na PBPA ni sehemu muhimu ya mkakati wa taifa wa kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya mafuta kwa uhakika na kwa manufaa ya wananchi," alisema Mheshimiwa Mwanaasha.

Aidha, alitoa wito kwa PBPA kuendelea kuimarisha ushindani na uwazi katika zabuni za uagizaji wa mafuta ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi na kuongeza ufanisi katika sekta hiyo nyeti kwa uchumi wa nchi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mheshimiwa Queen Sendiga, naye alitembelea banda la PBPA na kutoa pongezi kwa wakala huo kwa kutekeleza majukumu yake kwa weledi, uzalendo na kuzingatia maslahi mapana ya taifa.

"Elimu inayotolewa na PBPA kwa wananchi na wadau inaongeza uelewa kuhusu umuhimu wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja katika kudhibiti bei, kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa mafuta na kuimarisha uchumi wa nchi," alisema Mheshimiwa Sendiga.

Aliongeza kuwa jitihada za PBPA katika kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zimechangia kupunguza taharuki iliyokuwa ikijitokeza mara kwa mara pale bei za mafuta zinapobadilika, na badala yake kutoa nafasi kwa wananchi kuelewa uhalisia wa soko la kimataifa la nishati.

Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Zanzibar huwakutanisha wadau kutoka sekta mbalimbali za uzalishaji, biashara na huduma, yakilenga kukuza uchumi, uwekezaji na ubunifu.

Ushiriki wa PBPA katika maonesho hayo unaendelea kuthibitisha dhamira ya Serikali ya kuimarisha usimamizi wa sekta ya mafuta kupitia mifumo ya kisasa, shirikishi na yenye kuzingatia uwazi kwa manufaa ya taifa kwa ujumla.




***Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mhe. Mwanaasha Khamis, akiwa katika banda la Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) katika Maonesho ya 12 ya Kimataifa ya Biashara ya Zanzibar (ZITF) yaliyofanyika katika viwanja wa Dimani, Zanzibar.***




Wataalamu kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakitoa elimu kuhusu majukumu ya PBPA kwa wananchi waliotembelea Banda la ofisi hiyo katika maonesho ya 12 ya Biashara ya Kimataifa ya Zanzibar (ZITF) yaliyofanyika katika viwanja vya Dimani, Zanzibar.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Ofisi ya Zanzibar, Bw. Masoud Faki Mbwete akiwa katika banda la Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwenye Maonesho ya 12 ya Kimataifa ya Biashara ya Zanzibar (ZITF) yaliyofanyika katika viwanja vya Dimani, Zanzibar.





**Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA)**
**Sanduku la Posta 2634,**
**Dar es Salaam, Tanzania,**
**info@pbpa.go.tz.**
**+255 222 129 009**

PbpaTanzania PbpaTanzania pbpa_tanzania